

## Wafugaji watoe ushirikiano katika utambuzi wa mifugo

SERIKALI imekuwa ikitekeleza mpango wa kuvisha mifugo hereni za kieletroniki ambapo hadi kufikia Oktoba 15 mwaka huu, jumla ya mifugo milioni 4.2 ilikuwa imewekwa hereni hizo za utambuzi ikiwa sawa na asilimia 10 ya mifugo.

Lengo la serikali ni kuweka alama za utambuzi kwa mifugo milioni 45.9 kwa mchanganuo wa ng'ombe milioni 23.1, Mbuzi milioni 16.8, Kondoo milioni 5.6 na punda 420,000.

Katika mpango huo, Mkoa wa Mbeya unaongoza kwa kutambua mifugo 1,014,569 ukifuatiwa na Tabora yenye mifugo 440,133, Rukwa 354,895, Katavi 278,865 na Kagera mifugo 277,077 imetambuliwa kupitia mpango huo.

Hata hivyo katika utekelezaji wake, zimeibuka baadhi ya changamoto ikiwemo baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kutotenga fedha kwa ajili ya kuwezesha utambuzi huo.

Alitaja sababu nyingine ni kuchelewa kupatikana kwa kifungu cha utambuzi wa mifugo katika bajeti hivyo mamlaka kushindwa kutekeleza mpango huo kwa wakati.

Sababu nyingine kuwa ni baadhi ya wafugaji kulalamikia bei elekezi ya sh. 1,750 kwa hereni za ng'ombe, punda na sh. 1000 kwa mbuzi na kondoo.

Pia, sababu nyingine inayokwamisha zoezi hilo ni uelewa na mitazamo hasi kwa baadhi ya wafugaji kuhusu hereni za utambuzi pamoja na ukame ambapo katika kipindi cha Julai mwaka jana na Januari mwaka huu ulisababisha mifugo kuathilika.

Hata hivyo ni muhimu kwa jamii ya wafugaji kutambua kwamba hereni za utambuzi wa mifugo zinatumiwa kuonyesha utaifa wa mifugo, namba za mkoa, namba za mamlaka za serikali za mitaa na namba zinazoonyesha taarifa za mfugo na mfugaji.

Namba hizo hutolewa na serikali ambapo taarifa zake hutunzwa kwenye "barcode" ambazo hupatikana duniani kote kwa mfumo wa kielektroniki.

Ifahamike kwamba mfumo huo utawezesha kudhibiti matukio ya wizi wa mifugo kwani itakuwa rahisi kwa mifugo kutambulika mahali walipotokea na hata serikali kupata idadi kamili ya mifugo iliyopo katika kila eneo nchini.

Hivyo, wafugaji ni muhimu wakatoa ushirikiano wa kutosha kwa maofisa wa serikali wanaoendesha zoezi hilo kuhakikisha kwamba mifugo yao yote inatambuliwa na kuvishwa herein hizo maalum.